*Review Article*

*Section: Literature, Languages and Criticism*

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 5th April 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# The role of autobiographies and biographies in the promotion of Kiswahili prose

**John M'Raiji**
Masinde Muliro University of Science and Technology
Email: jmraiji@mmust.ac.ke
https://orcid.org/0000-0003-0935-6719

## Abstract

Despite the fact that Kiswahili prose has grown and made great strides as well as demonstrating high artistic levels through stylistic experimentations as well notable developments in content and presentation; some of its sub-genres especially the autobiographies and biographies seem to be overlooked by writers and literary critics in Kiswahili and thus they continue lagging behind as mediums of artistic expression. This article (re) evaluates and explains the role of these writings in the promotion of Kiswahili language and literature with an aim of rekindling enthusiasm in its composition and promotion as a feature of cultural development. The paper takes a theoretical perspective in that it evaluates a Kiswahili literary sub-genre from a historical perspective. The evaluation used critical analytical methods to examine the autobiographies and biographies in Kiswahili as well as to question and to evaluate the prevailing situation. Finally, the paper recommends that strategies for composing and teaching Kiswahili autobiographies and biographies be put in place in order to broaden their scope.

**Keywords:** autobiography, biography, Kiswahili, Kenya, prose

## How to Cite:

M'Raiji, J. (2021). The role of autobiographies and biographies in the promotion of Kiswahili prose. *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, 2(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/languages-and-literatures/article/view/580

**Public Interest Statement**

The use of critical analytical methods to examine the biographies and autobiographies, as literary expressions, promotes life-long learning and reading culture among adults.

© 2021 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 5th April 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# Nafasi ya tawasifu na wasifu katika ukuzaji wa nathari ya Kiswahili nchini Kenya

**John M'Raiji**
Masinde Muliro University of Science and Technology
jmraiji@mmust.ac.ke
https://orcid.org/0000-0003-0935-6719

**Ikisiri**

Licha ya kuwa nathari ya Kiswahili imekua na kupiga hatua kubwa za kimaendeleo pamoja na kudhihirisha ukwasi wa hali ya juu kupitia majaribio ya kimtindo pamoja na upevu wa kimaudhui; baadhi ya tanzu zake zikiwemo tawasifu na wasifu zinaonekana kupuuzwa na hivyo kubaki nyuma (Walibora, 2014). Hili linaonyesha kwamba tanzu za nathari ya Kiswahili kama vile riwaya, hadithi fupi na ushairi zimepanuka na kukua kuliko tanzu za tawasifu na wasifu hivyo kudhihirisha kuwa kazi za kinathari za Kiswahili hazijakua kwa viwango sawa kimtindo, kimaudhui na ki-idadi. Makala haya yanaeleza nafasi ya tawasifu na wasifu katika kukuza lugha na fasihi hii kutokana na hali inayoonekana kulemaza baadhi ya vipera vya nathari kwa jumla. Aidha matini hii ni upekuzi wa kinatharia na kitahakiki kutokana na hali kwamba inatathmini tanzu za kinathari za Kiswahili kwa mtazamo wa kihistoria. Hili ni kusema kwamba utafiti ulitumia mbinu za kiupembuzi kuchunguza mapisi ya wasifu na tawasifu za Kiswahili pamoja na kuhoji hali ya sasa ya utanzu huu chipukizi. Aidha umuhimu wa tawasifu na wasifu hasa katika kudumisha usomaji miongoni mwa watu wazima hasa baada ya kumaliza masomo ya shuleni unasisitizwa. Fauka ya hili, matini hii inapendekeza kuwepo mikakati na mustakabali wa kimakusudi wa kutunga na kufundisha tawasifu na wasifu shuleni ili kuupanua utanzu wa nathari zaidi. Swali linalobakia ni iwapo sera Madhubuti inaweza kuhimizwa katika kutekeleza mradi wa aila hii.

**Maneno muhimu:** Nathari, Wasifu, Tawasifu, Kiswahili, Kenya

## Utangulizi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:25), nathari ni tungo zinazotumia maelezo ya mfululizo au lugha ya mjazo kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji. Yaani ni utungo wowote ule unaotoa hadithi au usimulizi kwa kutumia "lugha ya mjazo au nathari ya mtiririko." Aidha nathari ya mtiririko ni maandishi yasiyo ya kishairi na ambayo hujidhihirisha kupitia tanzu za lugha ya kimaelezo. Baadhi ya mifano ya kazi za kinathari ni insha za kifasihi, novela, riwaya, hadithi fupi, barua, kumbukumbu, tarekhe, tawasifu na wasifu. Tungo za kinathari zinaweza kuwa za kifasihi ama zisiwe za kifasihi. Nathari za kifasihi ni bunilizi zilizotungwa kutokana na ubunaji wa mwandishi ilhali zisizo za kifasihi ni nathari zinazoelezea matukio ya kihistoria au kumbukumbu za kimapisi. Kutokana na maelezo haya, inahalisi kwamba nathari ni maandishi ya moja kwa moja ambayo si ya kishairi.

Utafiti wa awali unaonyesha kwamba nathari ya Kiswahili ina historia ndefu inayotokana na fasihi simulizi pamoja na utamaduni mkongwe wa uandishi wa Kiswahili. Isitoshe, nathari ni moja kati ya tungo za Kiafrika zinazokua kwa haraka (Mulokozi, 1985; 1992). Mulokozi anashikilia kuwa licha ya kwamba nathari ya Kiswahili imekua na kupiga hatua kubwa za kimaendeleo pamoja na kudhihirisha ukwasi wa hali ya juu kupitia majaribio ya kimtindo pamoja na upevu wa kimaudhui; baadhi ya tanzu zake zikiwemo wasifu na tawasifu; zinaonekana kupuuzwa na hivyo kubaki nyuma. Hili linaonyesha kwamba tanzu za nathari ya Kiswahili kama vile riwaya, hadithi fupi na ushairi zimepanuka na kukua kuliko tanzu za tawasifu na wasifu na hivyo kudhihirisha kuwa kazi za kinathari za Kiswahili hazijakua kwa viwango sawa kimtindo, kimaudhui na ki-idadi.

Historia ya uandishi kwa lugha ya Kiswahili unashahidia kwamba mtagusano wa karne nyingi baina ya Waswahili na wageni kutoka Uarabuni na nchi za Kimagharibi ulirutubisha uandishi wa kazi za kinathari kwa kutumia hati ya Kiarabu na baadaye kwa kuzingatia hati ya Kirumi. Hata hivyo haijabainika wazi ni kwa nini baadhi ya tanzu zilinawiri huku tawasifu na wasifu zikidorora nyuma. Aidha tanzu hizi 'tasa' hazina dafina kubwa ya maandishi kwa maana kwamba maandishi yake ni machache ikilinganishwa na tanzu nyinginezo katika uandishi wa Kiswahili. Isitoshe, tawasifu na wasifu hazijapanuka wala hazifundishwi sana shuleni na vyuoni ikilinganishwa na zilizotanda kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Tawasifu na wasifu za Kiswahili pia hazijakubalika pakubwa miongoni mwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili nchini Kenya na hivyo zinaelekea kulemaa na kukua pole pole sana. Kutokana na hali hii tatanishi, Makala haya yanahoji hali, historia na utunzi wa tawasifu na wasifu za Kiswahili na kutathmini nafasi yazo katika kukuza nathari ya Kiswahili. Aidha ninazingatia historia ya nathari nchini Kenya na kisha kudadisi nafasi yake katika karne ya ishirini na moja. Baadhi ya mapendekezo yanayotewa ni pamoja na kuwahamasisha waandishi, watunzi, walimu na wachapishaji kutilia mkazo uandishi, ufundishaji na usomaji wa tawasifu na wasifu katika viwango vyote vya elimu nchini Kenya.

Vigezo vya uainishaji wa nathari

Baadhi ya vigezo vinavyotumiwa kuainisha tungo za kinathari ni pamoja na jinsi lugha inayotumika, umbo la utungo, mtindo, pamoja na urefu wa maandishi yenyewe. Katika kiwango cha lugha, kila utanzu hutumia lugha kwa njia ya kipekee. Kwa mfano, ushairi wa kijadi wa Kiswahili hutumia lugha ya mkato ili kutosheleza kanuni za kiarudhi

hususan urari wa vina na wiano wa mizani. Kwa upande mwingine, tamthilia hutumia lugha ya mazungumzo na maigizo huku nathari ya riwaya na hadithi fupi zikizipambanua kutokana na masimulizi ya hadithi kwa lugha ya maelezo marefu yaliyopangwa katika aya na sura timilifu.

Inabainika kwamba katika kiwango cha umbo, kila utanzu huchukua sura yake dhahiri na ambao aghalabu huutofautisha na tanzu nyinginezo. Aidha upekee wa kiumbo huutambulisha utanzu mbali na kumtanabaisha msomaji kubainisha sifa zake za nje. Sifa za nje na zinazoonekana huupa utungo sura mahsusi inayoutambulisha na kuutofautisha kwa upevu unaokinaisha. Kwa mfano, tamthilia huumbwa na matukio na mazungumzo baina ya wahusika pamoja na kuigizwa kwenye jukwaa kwa mpangilio wa migawo ya maonyesho na/au vitendo. Kwa upande mwingine, ushairi wa kijadi hufuata mtiririko wa mishororo iliyopangwa kwenye beti. Kinyume na maumbo haya, riwaya hujikita katika mpangilio wa sura mbalimbali. Kwa upande mwingine, insha, barua na hadithi fupi huzingatia mpangilio wa aya bainifu.

Kigezo cha mtindo katika uainishaji wa tungo za kinathari aidha hutilia maanani swala la mbinu kuu inayotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe. Yamkini mbinu ya uwasilishaji katika fasihi huteuliwa kukidhi malengo au dhamira ya mtunzi. Kwa mfano, tamthilia huandikwa kwa ajili ya kuigizwa, kutendwa, au kuwasilishwa mbele ya hadhira ya jukwaani au kandamnasi. Kwa upande mwingine, ushairi hutungwa kwa madhumuni ya kuuwasilisha kwa njia na mahadhi ya ughanaji, ukaririwaji au uimbaji mbele ya halaiki. Pia shairi linaweza kuhifadhiwa akilini ya fanani kupitia maandalizi yanayomwezesha kulitenda bila kulisoma au akalisoma tu bila kulibaini kimoyomoyo. Isitoshe, shairi linaweza kutungwa tu kwa lengo la kulipua mihemko na hisia zinazombana mja ili kujiliwaza, kujifurahisha au kujikakamua kutokana na hali ya kibinafsi. Yaani linatungwa bila kulenga watu wengine bali 'kumponya' mtunzi kutokana na msongamano wa mawazo na jazba za Ndani kwa ndani.

Kinyume na sifa ziliyotajwa hapo juu, tanzu za riwaya, hadithi fupi, tawasifu na wasifu ni changamano zaidi kutokana na mbinu zake za uwasilishwaji kupitia maandishi yanayomlazimu msomaji awe na umilisi wa lugha fulani pamoja na ujuzi wa kusoma unaotokana na mafunzo au elimu: yaani shughuli ya usomaji ni matokeo ya mabadiliko makubwa yanayotokana na sayansi ya usomaji na uandishi. Aidha usomaji na uhakiki wa fasihi kwa jumla unahitaji umilisi mkubwa wa lugha pamoja na ufahamu wa michakato mbalimbali ya kinadharia na kifalsafa. Hata hivyo, mbinu za kiutanzu zinaweza kuingiliana, kuchangiana na kuathiriana. Kwa mfano, ushairi unaweza kutumiwa kwa malengo mbalimbali katika riwaya au tamthilia. Tawasifu na wasifu pia zinaweza kutumia vigeu vingenevyo kama vile picha, barua au maongezi ya simu kama ithibati ya maelezo na madai yake na hivyo kuzipa shani na upekee mbali na mawasilisho kupitia lugha nathari.

Kigezo cha mwisho kinachotumika katika kuainisha nathari ni urefu wa utungo ambao huibua; kwa mfano: tofauti baina ya novela na hadithi fupi. Swala la urefu wa nathari bado linazua mjadala miongoni mwa wataalamu. Iwapo hivyo, kila utanzu una matarajio na kanuni zake hivi kwamba riwaya ni ndefu kuliko novela kutokana na upeo, upana na udhabiti wa vipengele vinavyoshughulikiwa. Kwa mfano ushairi (ambao si kazi ya kinathari); una beti chache kuliko utenzi. Kwa upande mwingine, tawasifu na wasifu

mara nyingi hunasibishwa na kuainishwa kama riwaya kutokana na umbo pamoja na maelezo marefu yanayozingatia matumizi ya lugha ya mjazo iliyopangika katika aya na sura mbalimbali.

**Historia ya nathari ya Kiswahili**

Ushahidi unaonyesha kwamba tungo za mwanzo mwanzo za kinathari zilikuwa na athari ya mandhari ya Kiarabu. Kwa mujibu wa Rollins (1983), nathari za Kiswahili zilizoandikwa kabla ya 1800 mathalan tarekhe, kumbukumbu na wasifu zilidhihirisha athari za utamaduni na historia ya Kiarabu. Rollins anaendelea kueleza kuwa nathari hizo za awali aidha zilikuwa tungo fupi fupi zilizotokana na ukusanyaji wa masimulizi ya kimapokeo ambayo kiini chake ni utamaduni wa Waswahili lakini ulioathiriwa na mtagusano baina yao na Waarabu. Aidha simulizi hizo zilitokana na mapisi yaliyopitishwa, kuenezwa na kuhifadhiwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine na ambayo mwishowe yalinakiliwa kimaandishi hasa na wageni waliotangamana na Waswahili nyakati hizo.

Licha ya mwingiliano na Waarabu, Mulokozi (1993) anasema kwamba maandishi ya mwanzo kuhusu fasihi na nathari ya Kiswahili pia yaliasisiwa na wamishonari wa Kizungu wakiwemo Ludwig Krapf na Edward Steere katika karne ya 19. Wahubiri hawa walioishi Rabai na Unguja mtawalia aidha walikusanya mashairi, tenzi na ngano za kimapokeo na kuziandika kinathari hivyo kuweka msingi wa nathari ya Kiswahili. Hivyo basi, inahalisi kwamba maandishi ya kinathari yaliibuka kupitia msingi wa fasihi simulizi ya Waswahili. Kwa mfano, imerekodiwa kihistoria kwamba Edward Steere (1870) alikusanya hadithi za kimapokeo za Waswahili wa Unguja katika dafina ya Swahili Tales as told by the Natives of Zanzibar.

Mulokozi (1993) anaeleza kuwa baadhi ya wataalamu wengine wa kigeni walichangia nathari ya Kiswahili kwa kukusanya ngano za kimapokeo za Waswahili pamoja na za Waafrika wengine. Hao ni pamoja na Alice Werner aliyefanya utafiti kwa minajili ya shahada ya Uzamifu na kuandika kitabu Myths and legends of the Bantu (1932). Nathari nyinginezo za aula hiyo ni pamoja na za C. Velten, G. Buttner, K. Meinhof, Lyndon Harries, W. Whiteley, J.W.T. Allen, E. Dammann na H.E Lambert miongoni mwa wengine. Kazi za wataalamu hawa hazikuwa za kibunifu bali mikusanyiko ya fasihi simulizi ya Waafrika na ambayo waliiandikia kwa lugha nathari. Fauka ya hayo na kwa mintaarafu Mulokozi (1993), tarekhe ya nathari ya Kiswahili inabainisha kuwa maandishi mengi ya kinathari ya kati ya miaka ya 1840 hadi 1970 yalifanywa na wageni kwa ajili ya mahitaji yao pamoja na kwa niaba ya wageni wenzao na aghalabu kazi hizo ziliandikwa kwa lugha za kigeni; hasa Kiingereza na Kijerumani.

Rollins (1983) anasimulia kuhusu tungo za wamishonari zilizoandamana na nathari nyingezo za awali na ambazo haijulikani wakati wa kutungwa kwake: mathalani Safari yangu na bara Afrika iliyoandikwa na Selemani bin Mwenye Chande kuelezea ziara zake katika sehemu mbalimbali za Bara la Afrika. Nathari ya Safari yangu ya Urusi na ya Siberia iliyotungwa na Salim bin Abakari pia ilisimulia tajriba za mwandishi alipozuru Urusi na Saiberia. Rollins anadai kuwa licha ya kwamba kazi ya Salim bin Abakari inasimulia kuhusu safari za mtunzi kuliko maisha yake na hivyo kujinasibisha zaidi na tarekhe kuliko tawasifu

au maisha ya mtunzi; ina sifa kadha za kitawasifu kama vile upenyezi wa kitafakuri na kisaikolojia. Ibainike kwamba mojawapo ya sifa za tawasifu ni udadisi wa ndani kwa ndani wa saikolojia ya mtunzi kwa lengo la kuhalalisha tabia na misukumo ya matendo yake.
Kwa mujibu wa Rollins (ibid), mojawapo ya nathari nyingine ya awali katika lugha ya Kiswahili ni Maisha iliyotungwa na Hamed bin Muhamad el-Murjebi almaarufu Tippu Tip. Nathari hii inahusu maisha ya Tippu Tip aliyeishi Unguja. Tippu Tip alikuwa mashuhuri kutokana na tajriba yake kubwa ya kibiashara, kiutawala, kivita na kiupelelezi. Kutokana na ujuzi wa mfanyabiashara huyu kuhusu visiwa na bara, Tippu Tip alichaguliwa kama akida wa Sultan Barghash wa Unguja kusimamia himaya yake kubwa iliyozagaa Tanganyika na Kongo.

Historia na tawasifu ya el-Murjebi zinashahidia kwamba aliwasaidia David Livingstone na Henry Stanley katika jitahada zao za uinjilishaji wa kueneza dini ya Kikristo. Pia aliwaelekeza wapelelezi hao kupenya janibu alizozifahamu vizuri kutokana na safari zake za tangu ujana wake. Nathari ya el-Murjebi aidha inaanzia kwa kueleza wasifu wa alivyojiunga na misafara ya biashara katika maeneo ya bara akiandamana na ndugu yake anapoandika:

> Nilipopata miaka thenashara, nalishika safari za karibu.
> Hafanza biashara ya sandarusi, na [… ]
> pamoja na ndugu yangu... (Maisha, 8).

Mbali na kazi za kinathari zinazoelezea maisha ya watu binafsi, tungo za awali za Kiswahili pia zina kumbukumbu na tarekhe za kihistoria. Kwa mfano, Tarekhe ya Pate iliyoandikwa na Fumo Omar al-Nabhani katika karne ya 19 inaeleza historia ya Kisiwa cha Pate katika karne za 18 na 19.

Kazi hizi za awali kwa pamoja zinadhihirisha kwamba tawasifu ya Kiswahili iliwekewa msingi wa kuigwa na watunzi wa baadaye hata kabla ya tungo za Shaaban Robert. Waaidha, watunzi wa jadi waliweka msingi wa tungo za kinathari uliowahamasisha wenyeji akiwemo Shaaban Robert. Hata hivyo, nathari za Kiswahili zinazotambulika zaidi nchini Kenya ni riwaya na hadithi fupi.

Riwaya na hadithi fupi ni maarufu kutokana na wingi wake pamoja na mikakati ya kinadharia iliyowekwa kuzihakiki na kuzifundisha hasa katika shule za upili na vyuo. Hata hivyo, wanafunzi wengi wa Kiswahili nchini Kenya hawafamu mengi kuhusu tawasifu na wasifu za Kiswahili. Udhaifu huu unajitokeza katika fasihi ya Kiswahili licha ya kwamba utunzi wa kumbukumbu, tarekhe, insha, tawasifu na wasifu ulitangulia uandishi wa riwaya na hadithi fupi za Kiswahili.

Kazi ya kinathari inayosemekana kuwa ya kwanza katika Kiswahili ni Habari za Wakilindi kilichoandikwa na Abdallah bin Hemedi bin Ali Ajjemy (1895; 1907) . Habari za Wakilindi ni kitabu kinachosimulia kuhusu himaya ya Kilindi na watawala wa Usambara. Hivyo basi kuna ushahidi kwamba nathari ya kwanza ya Kiswahili ni riwaya ya kihistoria au tarekhe wala sio tawasifu na wasifu. Kwa mfano Shaaban Robert alichangia sana nathari ya kitawasifu kwa kuweka msingi imara kupitia tungo zake. Kareithi (1969) katika Kaburi bila

Msalaba anaeleza kuhusu vita vya Mau Mau. Kazi hii inaonyesha dhuluma waliyofanyiwa Waafrika na wakoloni na hivyo kuhifadhi sehemu ya historia ya Kenya sawa na alivyofanya Bernard Mapalala (1992) alipoeleza kuhusu utawala wa mtemi Mirambo kutoka Tanzania katika Kwaheri Iselamagazi.

**Fasili ya wasifu na tawasifu**

Kwa mujibu wa Paneli la Kiswahili (2018), wasifu ni maelezo ya kina kuhusu maisha, matendo na tabia ya mtu tangu kuzaliwa kwake. Masimulizi ya kiwasifu aidha huandikwa na mtu mwingine anayeyafahamu au kuyatafitia bali si mhusika mwenyewe. Wasifu huelezwa na kufafanua mambo ya kimsingi kuhusu ukuaji, elimu, kazi na ujuzi wa mtu mashuhuri. Kwa mfano, kuna watunzi mbalimbali walioandika wasifu za watu maarufu; mathalan wasifu wa Mzee Jomo Kenyatta (Kenya), wasifu wa Barack Obama (Marekani), wasifu wa Nelson Mandela (Afrika Kusini) au wasifu wa Julius Nyerere (Tanzania).

Wasifu unaweza kuwa umeithinishwa au haujaithinishwa rasmi ila kimsingi, anayeandika wasifu ni tofauti na anayezungumziwa katika wasifu huo. Kwa mfano katika Wasifu Wa Siti Binti Saad, Shaaban Robert (1958) anasimulia kuhusu maisha ya Siti Binti Saad, mtribu maarufu kutoka Unguja aliyeishi baina ya 1880 na 1950. Saad alikuwa "mwanamke wa kwanza Zanzibar kusimama jukwaani na kuimba nyimbo za taarab." (Robert, 1991: i).

Kwa upande mwingine, Paneli la Kiswahili (2018) inaieleza tawasifu kama masimulizi ya mtu binafsi kuhusu maisha yake mwenyewe. Tawasifu aghalabu husimuliwa katika nafsi ya kwanza. Tawasifu vile vile huangazia kipindi fulani tu cha maisha ya mtunzi wala si lazima kushughulikia tangu kuzaliwa hadi kufa. Kwa mfano tawasifu za Shaaban Robert, Maisha yangu (1936) na Maisha yangu na baada ya miaka hamsini (1969) ni tawasifu mbili kuhusu maisha yake mwenyewe. Tawasifu ya kwanza ya Shaaban Robert ilikuwa insha iliyoshughulikia maisha yake ya utotoni na ambayo yamkini ilishinda tuzo na pia ikachapishwa katika gazeti mojawapo la wakati huo. Katika Maisha yangu na baada ya miaka hamsini, swala la tawasifu yake ya awali na ambayo haipatikani kama kitabu linaelezewa ifuatavyo:
Miaka kumi imepita tangu mwandishi wa kitabu hiki [Shaaban Robert] alipoandika insha juu ya maisha yake mwenyewe iliyosimulia kwa muhtasari utoto, michezo, vyuo, kumbi, utu uzima, kazi na arusi. Insha yake ilifaulu ikapata tuzo ya kwanza katika shindano la kuandika insha lililofanywa Afrika Mashariki katika mwaka wa 1936. (Robert, 1936: utangulizi)

Ingawa hakuna nakala yoyote ya tawasifu ya kwanza ya Shaaban Robert (Walibora, 2014), ile ya pili ina toleo kadha baada ya chapisho la kwanza na aidha imechangia pakubwa kuweka msingi wa tawasifu za Kiswahili na hivyo kuwahamazisha watunzi wa baadaye.

Baadhi ya maswala anayoshughulikia katika Maisha yangu na baada ya miaka hamsini kutokana na tajriba ya maisha yake ni pamoja na utu, utajiri na matumizi ya pesa, sifa za mwanamke, watoto wake, mke wake wa pili, kazi na taaluma yake, umuhimu wa elimu, utunzi wa ushairi, siasa, matumizi ya lugha (ya Kiswahili) miongoni mwa maudhui mengineyo. Tawasifu za Shaaban Robert zinajikita katika mpangilio wa kijamii, kihistoria na kisiasa kabla na baada ya uhuru wa Tanganyika hasa tunapotilia maanani kwamba wasifu na tawasifu ni sanaa na historia kwa wakati mmoja hasa kutokana na mandhari yaliyomzunguka mtunzi. Tofauti na bunilizi, wasifu na tawasifu hujikita katika mazingira

halisi ya kijamii na kitaifa na hivyo husheheni ukweli mwingi wa kimapisi.

Uteuzi na matumizi ya lugha katika wasifu na tawasifu pia ni kipengele muhimu katika kupitisha ujumbe. Si rahisi kutofautisha bunilizi na tawasifu au wasifu kwa kuzingatia kigezo cha matumizi ya lugha kutokana na ukweli kwamba tanzu zote hudhamiria kuifinyanga lugha upya na hususan kuitumia kama nyenzo ya kugusa na kuacha athari za kisanaa kwa wasomaji. Watunzi wa wasifu na tawasifu hawana budi kutumia lugha yenye mvuto, shani au ufundi wa kisanaa ili kukithi mionjo ya wasomaji. Kwa mfano, Shaaban Robert anatumia mbinu na lugha nyoofu zinazoifanya nathari zake kutajwa miongoni mwa tawasifu bora katika lugha ya Kiswahili (Mtanga, 2018) na hivyo kudhihirisha kwamba wasifu na tawasifu zinaweza "kuibua ubora wa kisanii lakini pasipo kujitenga na […] kweli ya kitawasifu" (2014, viii).

**Usomaji na utunzi wa wasifu na tawasifu nchini Kenya**

Kulingana na NOP World Culture Score Index, Wakenya hawana uzoefu wa kusoma hasa baada ya kumaliza shule. Kulingana na utafiti huo, India ndio nchi yenye kiwango cha juu kabisa cha usomaji ikifuatwa na Thailand na Uchina. Misri na Afrika Kusini aidha zinaorodheshwa kama nchi za Kiafrika zilizo na kiwango cha juu Zaidi (Examined Existence Team 2, 2021). Hali hii inaonekana kuchangiwa na mashirika ya uchapishaji wa vitabu kwa kupendelea kuchapisha vitabu vya matumizi ya shuleni kuliko vitabu ambavyo havina dalili ya kuteuliwa kusomwa shuleni.

Swala hili linaonekana kukubalika kwani waandishi na wachapishaji wanategemea faida kutokana na mauzo ya vitabu wanavyovitoa. Licha kwamba tafiti zinaonyesha kuwa Wakenya wengi hawasomi baada ya kutoka shuleni, tawasifu na wasifu chache zilizochapishwa nchini zimeshabikiwa na kununuliwa na watu wazima. Kwa mfano, Not Yet Uhuru, tawasifu ya Jaramogi Oginga Odinga iliyochapishwa mara ya kwanza mwaka wa 1967 imetolewa na makampuni tofauti tofauti takriban mara kumi na moja tangu ilipochapishwa. Huu ni ushahidi kwamba Wakenya hupendwa kusoma wasifu na tawasifu nzuri.

Mifano ya baadhi tu ya wasifu na tawasifu zinazopendelewa na Wakenya ni kama vile Beyond expectations: From charcoal to gold (Njenga Karume, 2009), Unbowed: A memoir (Wangari Maathai, 2006), Dreams in a time of war: A childhood memoir (Ngugi wa Thiong'o, 2010) na Raila Odinga: An enigma in Kenyan politics (2006) pamoja na nyinginezo za kigeni kama vile Long Walk to Freedom (Nelson Mandela, 1995), Dreams from my father & The audacity of hope (Barack Obama, 1995; 2016) na Becoming (Michelle Obama, 2018) ni miongoni mwa nathari maarufu nchini Kenya. Hili linadhihirisha kwamba Wakenya husoma nathari za kimaisha licha ya kwamba zimeandikwa kwa Kiingereza. Kuna uwezekano kuwa wangezisoma za Kiswahili kama zingekuwepo au iwapo wangehamasishwa kupitia mfumo wa elimu kukienzi Kiswahili.

Vitabu hivi, na vingenevyo vingi, vinauzwa sio tu kwenye maduka rasmi na mtandaoni bali pia kwenye barabara za miji mikuu ya Kenya. Isitoshe, baadhi ya nathari hizi zimechapishwa katika magazeti maarufu kama vile Daily Nation hivyo kusisitiza kuwa Wakenya husoma wasifu na tawasifu japo hupendelea zilizoandikwa kwa Kiingereza.

Utunzi, usomaji na ufundishaji wa nathari za wasifu na tawasifu utaendeleza, kukuza, kuboresha na kurutubisha fasihi ya Kiswahili (Walibora 2014, xi). Ni muhimu kwa magazeti kuchangia usomaji wa wasifu na tawasifu za Kiswahili mithili ya ilivyokuwa Shaaban Robert alipotunga tawasifu yake ya kwanza.

Ushahidi unathibitisha kwamba asimilia kubwa ya magazeti na majarida nchini Kenya huandikwa kwa Kiingereza. Mojawapo ya sababu za Wakenya kupendelea matini za Kizungu ni kwamba mfumo wa elimu pamoja na sera ya lugha zinapendelea matumizi ya Kiingereza. Yaani Kiingereza nchini Kenya sio tu lugha rasmi na ya taifa kando na Kiswahili bali pia ni lugha ya kufundishia masomo mengine yote isipokuwa Kiswahili chenyewe. Fauka ya hayo, Kiingereza, hunasibishwa na usomi, kazi nzuri, hadhi kubwa, teknolojia, pamoja na ukwasi wa kiuchumi. Aidha Kiingereza huonewa fahari kinyume na Kiswahili ambacho hutumiwa katika mawasiliano ya kawaida pamoja na maingiliano baina ya watu wa makabila mbalimbali. Si ajabu basi kukumbana na Wakenya wanaoweza kuzungumza na kuelewa Kiswahili lakini hawana umilisi wa kusoma wala kuandika makala kwa Kiswahili. Vyombo vingi vya habari na matangazo hutegemea matumizi ya Kiingereza. Habari kwenye redio na televisheni zenye ushawishi mkubwa mathalani vituo vya Nation TV na redio, Citizen TV na redio, KTN News na K24: hupeperushwa nyakati zenye watazamaji wengi. Matokeo ya mapendeleo haya ni kuimarishwa kwa kasumba na hisia hasi dhidi ya Kiswahili. Kuna baadhi ya Wakenya wanaochukulia kwamba mtu anayesoma gazeti la Kiswahili kama Taifa Leo ni asiyemudu kusoma Kiingereza na hivyo hajaelimika kwani watu wengi hunasibisha elimu na lugha ya Kiingereza.

Utunzi, usomaji na ufundishaji wa nathari za wasifu na tawasifu utaendeleza, kukuza, kuboresha na kurutubisha fasihi ya Kiswahili (Walibora, xi). Kuna haja ya kubadilisha mtazamo huu potofu iwapo soko la wasifu na tawasifu za Kiswahili, na hivyo utunzi wake; utaimarishwa. Utunzi, ufundishaji na usomaji wa wasifu na tawasifu za Kiswahili unaweza kutatajirisha fasihi ya Kiswahili. Aidha mikakati ya kufaulisha mradi wa kukuza wasifu na tawasifu za Kiswahili inapaswa kuwekwa na kuendendeleza na vyombo vya habari nchini. Baadhi ya sababu za watu wazima kuchangamkia wasifu na tawasifu ni udadisi, udaku au shauku ya kutaka kujua wanavyoishi watu mashuhuri. Aidha wasifu na tawasifu husheheni visa vya ushindi na majuto kwa upande mmoja, lakini husawiri ushindi au mafanikio ya wahusika kwa upande mwingine; na hivyo kuwapa moyo wasomaji kwa kuwadhihirishia kwamba takriban waja wote hupitia maisha yenye changamoto bia. Aidha wasomaji hujiliwaza, kuelewa, kuhisi na kulinganisha maisha yao na ya wahusika wa kitawasifu hasa wanapokumbana na kusuluhisha changamoto za kimaisha. Wasomaji pia hudhamiria kujifunza mengi kutokana na tabia na matendo ya wahusika wakuu wa kitawasifu kwa lengo la kuyaboresha maisha yao hususan kufikia ufanisi wa kiuchumi, kifedha, kiafya, kisiasa na kijamii.

Almuradi baadhi ya wasomaji huyafumbata maisha ya wahusika wakuu kama kielelezo cha kuiga au kujifunza kwani majagina wa wasifu na tawasifu hueleza shauku na shida walizokumbana nazo lakini hatimaye wakafaulu. Fauka ya hayo, wasomaji hudokezewa saikolojia au fikra za ndani zilizowasukuma wahusika kufanya maamuzi waliyoyafanya pamoja na kuangaziwa mitafaruku yao ya ndani kwa ndani walipokumbana

na maamuzi mazito. Aidha watu maarufu huelekeza matukio makubwa katika jamii zao na hivyo wanapaswa kuhimizwa kuandika au kuthamini utafiti na utunzi kuhusu maisha yao kukuza historia na utamaduni wa kitaifa. Licha ya changamoto zinazokumba uchapishaji katika mataifa yanayoendelea, watu waliofaulu maishani wana tajriba zinazoweza kumotisha wanajamii na hasa vizazi vilivyo nyuma (Gethoi, 2016).

Pia kuna haja ya shule za Kenya kufunza mbinu za uandishi wa wasifu na tawasifu kama taaluma ili kukuza kundi la waandishi bora wa wasifu. Utunzi ni utaalamu unaoweza kutumika kama kitega ajira mkabala na uhariri, utafsiri na ukalimani. Baadhi ya wamiliki wa wasifu pevu aidha hutumia waandishi wenye uzoefu mkubwa. Kwa mfano, tawasifu rasmi ya Steve Jobs aliyechangia uvumbuzi na matumizi ya teknolojia na mawasiliano kupitia tarakilishi alimrai mwandishi maarufu Walter Isaacson, ambaye pia ameandika tawasifu za Benjamin Franklin, Albert Einstein na Henry Kissinger: kuandika kuhusu maisha yake (Isaacson, 2011, 18).

Gethoi (2016) anaonelea kwamba kuna uhitaji wa kuandika tawasifu angavu na zilizotafitiwa vizuri kuhusu viongozi kama vile nchini Kenya kama vile Jomo Kenyatta, John Michuki, Paul Ngei, Askofu Henry Okullu, Mwai Kibaki na Charles Njonjo miongoni mwa wengine: kwa sababu tawasifu nzuri ni sehemu ya historia ya jamii anamotoka mhusika. Basi inasikitisha kwamba watunzi wengi wa tawasifu na wasifu hulenga hadhira ya watu wazima hivi kwamba baadhi ya nathari hizi pevu haziwavutii wanafunzi wa shule za upili na sekondari kwa sababu kiwango cha lugha katika nathari hizo unalenga wasomaji wenye elimu ya juu.

Changamoto ya utunzi unaolenga hadhira ya watu wazima na wasomi ni kwamba vijana wengi wasio na uzoefu wala fursa ya kuzidurusu nathari zenye maelezo mengi ya kihistoria, kitaaluma na kifalsafa wataendelea kukosa natija iliyomo katika tawasifu na wasifu. Licha ya kikwazo hiki pamoja na ughali wa vitabu hivyo, wasifu na tawasifu hazifundishwi katika shule za msingi wala za sekondari nchini Kenya bali hufundishwa kama kozi ya hiari katika baadhi ya vyuo vikuu hasa kwa wanafunzi wanaosomea fasihi ya Kiingereza au Kiswahili. Fauka ya hili, kuna uhitaji wa tungo zaidi katika lugha zote mbili ili kujenga wataalamu wa kutafiti na kuziandika kazi nzuri zinazolenga wasomaji wachanga na waliokomaa.

Buhere (2018) anasisitiza kwamba kuna haja ya kutunga wasifu nyepesi na fupi zinazolenga hadhira ya watoto badala ya kuandikia tu hadhira ya watu wazima peke yake. Aidha watunzi wa Kiswahili wanapaswa kuandika nathari fupi na zinazotumia lugha na mitindo inayovutia na kueleweka kwa urahisi na hadhira ya watoto na vijana. Pendekezo hili ni muafaka hasa tukizingatia kwamba wasifu na tawasifu nyingi nchini Kenya aidha ni za kigeni na zinazolenga hadhira ya watu wazima. Usomaji wa nathari za aula hii katika umri mdogo utakuza ari ya kutaka kusoma zaidi pamoja na kuwapa watoto na vijana vielezo vizuri vya kuiga maishani mwao. Kwa mfano, watoto wa kike wanaweza kutiwa hamu ya kuwaiga akina mama waliofaulu katika nyanja mbalimbali za kitaaluma na kiutendakazi na hivyo kuchangia uimarishaji wa usawa na haki za kijinsia.

**Utasa wa wasifu na tawasifu za Kiswahili nchini Kenya**

Ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili ulianza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nchini Tanzania mwaka wa1968 na mnamo 1980 katika Chuo Kikuu cha Nairobi nchini Kenya. Hata hivyo, na licha ya kielelezo cha Shaaban Robert na baadhi ya waandishi waliomtangulia; utunzi wa wasifu na tawasifu za Kiswahili umepiga hatua ndogo sana kutoka miaka ya 70 hadi sasa. Hili ni jambo la kusikitisha hasa kwa sababu Kiswahili kimefundishwa katika shule za msingi, za upili na vyuoni vya Tanzania na Kenya tangu mataifa haya yalipopata uhuru. Walibora (2014, ix) anasikitikia utasa huu kwa kusema kwamba "ni waandishi wachache mno wa bunilizi za Kiswahili waliowahi kuandika kuhusu maisha yao-ya utotoni na ukubwani." (Walibora, 2014, ix).

Utasa wa wasifu na tawasifu za Kiswahili aidha ungali upo licha ya kwamba uchambuzi na uhakiki wa fasihi ya Kiswahili uliongezeka baada ya nchi hizi kupata uhuru. Wasifu na tawasifu hazijapanuka kama tanzu za riwaya, hadithi fupi, tamthilia au ushairi. Bunilizi za Kiswahili zimekua kimtindo na kimaudhui kupitia tungo nyingi za upeo wa juu katika viwango vya kisanaa, kifani, kiuhalisia pamoja na za majaribio ya kiupembuzi. Riwaya za Shaaban Robert, Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohamed, Mohamed Said Mohamed, Kyalo Wadi Wamitila miongoni mwa wengine zimepanua bunilizi za Kiswahili kwa kutumia mitindo pevu inayoshabikiwa na wasomi wa vyuoni. Aidha maendeleo makubwa yamefikiwa katika ufundishaji, utunzi na uhakiki na tanzu zingine zote za fasihi ya Kiswahili isipokuwa wasifu na tawasifu.

Kwa mfano, riwaya za Euphrase Kezilahabi (katika Nagona na Mzingile), Said Ahmed Mohamed (katika Babu Alipofufuka) na Kyallo Wadi Wamitila (katika Binadamu! na Musaleo!) zimechangia katika kuikuza riwaya ya kisasa ya Kiswahili kupitia mtindo wa kimajaribio wa uhalisi-ajabu unaokiuka kaida zilizozoeleka za utungaji wa riwaya. (Kamis, 2003)

Kwa upande mwingine, utunzi wa ushairi wa kijadi umebadilika na kukubali utunzi huru usiozingatia kaida za vina na mizani zilizoutawala kwa miongo mingi. Baadhi ya washairi wa kumbo hili ni pamoja na Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Mabadiliko haya aidha yalizua mjadala uliochangia kuibua mitazamo pevu katika nadharia ya ushairi wa Kiswahili. Diwani nyingi za mashairi ya kiarudhi na yasiyo ya kiarudhi zimetungwa na kuinua kiwango cha taaluma ya fasihi kwa jumla. Utanzu wa hadithi fupi pia haukubaki nyuma kupitia mikusanyiko mingi ilhali wasifu na tawasifu zilizochapishwa katika kipindi hicho hicho ni chache mno.

Baadhi ya watunzi wa wasifu za Kiswahili baada ya Shaaban Robert katika miaka ya hivi karibuni ni pamoja na Amira Msellem aliyetunga Wasifu wa Sheikh Ahmed Nabhany (2012) kuhusu maisha ya marehemu Nabhany aliyekuwa mtaalamu wa lugha, utamaduni, mapisi na ushairi wa Kiswahili nchini Kenya. Tawasifu nyingine kutoka Unguja ni Mbali na nyumbani ya Adam Shafi (2010) ambayo inatongoa hamu ya mwandishi ya kusafiri kutoka kisiwani hadi nchi za mbali. Shafi anaeleza alivyofanikiwa kutimiza ndoto yake alipofunga safari ya meli kwenda kusoma Uingereza.

Aidha maisha ya msomi maarufu wa Kiswahili Shihabuddin Chiragdin yamesherehekewa kupitia wasifu ulioandikwa kwa lugha ya Kiingereza na mwanawe

Latifa S. Chiragdin (2012) katika Life journey of a Swahili scholar. Kitabu hiki kinapaswa kutafsiriwa kwa Kiswahili ili kuimarisha dafina ya nathari za Kiswahili na kwa heshima ya Chiragdin ambaye ametunga na kuhakiki mashairi pamoja na kuandika kuhusu historia ya Kiswahili.

Tawasifu nyinginezo ni pamoja na Nasikia Sauti ya Mama ya Ken Walibora (2014) inayoelezea maisha yake ya utotoni hadi alipoingia shule ya upili. Walibora anasistiza kwamba aliitunga tawasifu hii kama "changamoto… kwa waandishi wengine wa buninilizi za Kiswahili pia wajitose katika utanzu huu muhimu sana katika fasihi ya Kiswahili (Walibora, 2014, xi). Ni jambo la kutia moyo na matumaini kwa wawashikadau wa Kiswahili mtangazaji, mtunzi na msomi huyu anapoahidi wasomaji wake kwamba ataandika "tawasifu nyingine vile vile kuhusu maisha [yake] ya ukubwani, au hata zaidi ya tawasifu moja ikibidi kwa kufuata nyayo za watangulizi" wa awali kama vile Wole Soyinka aliyeandika tawasifu tatu kuhusu maisha yake (Walibora, xi).

Nafasi ya tawasifu na wasifu katika ukuzaji wa nathari ya Kiswahili katika karne ya 21 Usemi wa Walibora (2014, xi) kwamba ingawa karne ya ishirini na moja "inaitwa karne ya tawasifu [lakini] Kiswahili bado tuko nyuma" una mashiko hasa tupozingatia kwamba dhana ya ujifunzaji maishani imependekezwa ulimwengu mzima. Kwa mujibu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamadunila la Umoja wa Mataifa, (UNESCO) mkakati wa kujifunza maishani yote ni:

> "shughuli za kujifunza kwa kila kizazi katika miktadha yote (nyumbani, shuleni, jamii, mahali pa kazi, nk) na kutumia njia tofauti (elimu rasmi na isiyo rasmi) ambazo kwa pamoja hulenga mahitaji anuwai na yanayohusiana na kujifunza [...]
> Aidha kujifunza maisha yote ni mjadala wa kimataifa, kwa kuwa ni sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030 yanayozihimiza nchi kuhakikisha kuwepo kwa elimu bora, yenye usawa na jumuishi ili kukuza fursa ya kujifunza maisha yote kwa binadamu wote." (UNESCO, 2016: 2).

Dhana ya kujifunza maishani yote inarejelea masomo ya hiari na yanayoendelea maishani mwa mwanadamu kwa lengo la kujipatia maarifa ya kijumla au ya kitaaluma. Usomaji huu unatarajiwa kufaulisha mahusiano bora ya kijamii, ushiriki wa wananchi katika shughuli za kitaifa; pamoja na kudumisha ujuzi na utendakazi wa anayehusika. Aidha ujifunzaji maishani mwote humwezesha mhusika kushirikiana na walimwengu wengine licha ya tofauti zao za kimaumbile na kimaeneo. Dhana hii ni fahiwa inayohusisha watu wa kila umri ulimwenguni kote kupitia mifumo ya elimu iliyo rasmi na isiyo rasmi. Aidha elimu inayopendekezwa katika karne ya ishirini na moja ni isiyo na kikomo na inayomwezesha binadamu kupata ujuzi na maarifa zaidi hata baada ya kuhitimu shule. Mtazamo huu unatokana na ukweli kwamba binadamu anapaswa kujiendeleza kielimu na kiujuzi nyakati zote za maisha yake kutokana na mabadiliko pamoja na uvumbuzi mpya kila kuchao.

Mabadiliko ya kiutandawazi pamoja na teknolojia habari yanawalizimu binadamu

kujihami vilivyo ili kushiriki kikamifu katika shughuli zote za ulimwengu uliowazunguka. Teknolojia na mitagusano ya karibu baina ya walimwengu kutoka mataifa mbalimbali kupitia mitandao ya intaneti na mitandao ya kijamii, mahusiano ya kibiashara pamoja na mashirika ya kimataifa ni baadhi ya misukumo ya kuwepo elimu isiyo na kikomo.

Ulimwengu wa sasa umezua uhitaji wa kufahamu mambo mengi kupitia vyombo na mashine za kiteknolojia. Kwa mfano, vitabu-e almaarufu e-books vinachapishwa na kusambazwa kupitia intaneti na hivyo basi uzinduzi wa mbinu za kusambaza vitabu kupitia teknolojia, matumizi ya simu za mkono, tarakilishi, pamoja na matumizi ya vipakatalishi shuleni na vyuoni ni baadhi ya hatua zinazoweza kuepuka gharama kubwa ya uchapishaji, usafirishaji na ununuzi wa vitabu (Mungai, 2017; Kimani, 2019; Sachdev, 2019).

Aidha matini za kinathari zinaweza kutafsiriwa ili kuwafikia na kueleweka na watu wanaotumia lugha tofauti. Wasifu na tawasifu zilizoandikwa kwa Kiswahili zinaweza kutafsiriwa katika lugha nyinginezo kwa urahisi kuliko ilivyokuwa miaka michache iliyopita. Mojawapo ya bidhaa ambazo Kenya inaweza kuuza katika soko la kimataifa ni utamaduni wake ikiwemo vitabu na lugha kupitia tafsiri anuwai. Ubadilishanaji wa ujuzi pamoja na vifaa vya kiteknolojia umerahisishwa hasa kwa watu wenye ujuzi wa kutumia tarakilishi. Fauka ya faida zinazotokana na ufahamu na uelewa wa maswala-ibuka kama vile uvumbuzi mpya katika nyanja za kilimo, tiba, uwekezaji, pamoja na tasnia ya uzalishaji mali.

Katika hali namna hii basi, na tukizingatia kwamba watu wazima hupendelea kusoma wasifu na tawasifu, utunzi na tafsiri ya nathari za Kiswahili utaimarisha usomaji na ukuzaji wa ujuzi katika maisha yote ya binadamu mwenye shauku ya kujifunza maishani yake yote. Utunzi wa wasifu na tawasifu zinazopendelewa na watu wazima nchini Kenya utachangia kufanikisha mkakati huu wa Umoja wa mataifa.

## Hitimisho

Matini hii imedadavua hali ya tawasifu na wasifu za Kiswahili kwa kuzingatia chimbuko lake katika Karne ya 19. Aidha imeonyesha kwamba ukuaji wa nathari hizi mbili haujaendelea kama tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili licha ya kuchipuka kabla ya tanzu za riwaya na hadithi fupi. Sura hii pia imetetea ukati na umuhimu wa kutunga na kusoma tawasifu na wasifu katika kukuza fasihi ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja huku ikizingatiwa kwamba mwelekeo wa elimu ulimwenguni kote kwa sasa unalenga kuhakikisha ujifunzaji wa binadamu maishani yake yote wala sio kwa minajili ya kupita mitihani pekee. Aidha makala yameunga mkono usemi wa Walibora (2014) kwamba karne ya ishirini na moja ni karne ya utunzi na usomaji wa tawasifu na wasifu. Isitoshe, Makala haya yamechunguza historia na maendeleo ya nathari za kitawasifu kwa lugha ya Kiswahili na aidha kuonyesha udhaifu unaotokana na kutochangamkia baadhi ya nathari zake. Aidha changamoto za utunzi wa tawasifu na wasifu zimezingatiwa na mapendekezo ya kustawisha nathari hizi katika siku za usoni kutolewa. Mojawapo ya mapendekezo hayo ni ufunzaji wa tawasifu na wasifu katika shule za upili na vyuo nchini Kenya ili kuimarisha usomaji wa nathari miongoni mwa watu wazima.

**Funding:** This research received no external funding.

**Conflicts of Interest:** The authors declare no conflict of interest.

## Author Bionote

M'Raiji john Kirimi is an academician, researcher and cultural communication expert with vast experience both in Kenya and Botswana. M'Raiji holds a PhD in AfricanLanguages and Literature specializing in Kiswahili and Cultural Communication from theUniversity of Botswana. Dr M'Raiji has led teams and provided consultancy on communication and community development especially in the role and impact of modern communication and technology. His experience covers the teaching and application of language, literature and cultural communication strategies in transforming rural and urban livelihoods. M'Raiji is currently serving as a Senior Lecturer and researcher at Masinde Muliro University of Science and Technology in Kenya.

## Marejeleo

El-Murjebi. (1966). Maisha (Tafsiri. W. H. Whiteley). Nairobi: East African Literature Bureau.

Examined Existence Team 2. (2021). Readers Round the World: Where do people read more? https://examinedexistence.com/which-country-reads-the-most/

Buhere, K. (2018). The great educational tools that are autobiographies, biographies. Katika https://www.nation.co.ke/oped/letters/great-educational-tools-that-are-autobiographies-biographies/440806-4460590-Idgnuj/index.html

Gethoi, wa M. (2016). Want to write biography of a famous Kenyan? Good luck. Katika Daily Nation. https://www.nation.co.ke/lifestyle/weekend/Want-to-write-biography-of-a-famous-kenyan/1220-3287236-avpxjcz/index.html

Isaacson, W. (2011). Steve Jobs. New York. Simon & Schuster.

Kagita, A. (2015). Mbinu za kifani katika riwaya ya Mzingile ya E. Kezilahabi (1991). Katika http://kagitaibrah.blogspot.com/2015/05/uchambuzi-wa-fani-katika-riwaya-ya.html

Kareithi P. M. (1969). Kaburi bila msalaba: Hadithi ya vita vya Mau Mau. Nairobi: East African Publishing House.

Karume, N. (2009). Beyond expectation: From charcoal to gold. Nairobi: East African Educational Publishers.

Khamis, S. A. M. (2003). Fragmentation, orality and magic realism in Kezilahabi's novel Nagona. Nordic Journal of African Studies 12 (1): 78-91. 2003. http://www.njas.helsinki.fi/pdf-files/vol12num1/khamis2.pdf

Kimani, T. (2019). Kenya youths accessing online jobs through Ajira Digital Program. https://allafricayouths.com/2019/07/kenya-youths-accessing-online-jobs-through-ajira-digital-program/

Maathai, W. (2006). Unbowed: A memoir. New York: Alfred A. Knopf.

Mandela, N. (1994). Long walk to freedom. New York: Little Brown & Company.

Mtanga, F. (2018). Kitabu cha maisha yangu na baada ya miaka hamsini. Katika https://medium.com/@fadhymtanga/kitabu-cha-maisha-yangu-na-baada-ya-miaka-hamsini-85c78ca070ee

Mulokozi, M. M. (1992). A survey of Kiswahili literature: 1970-1988. Dar es salaam: Afrika Focus.

Mulokozi, M. M. (1985). The present state of Swahili literature: A survey. Katika Journal of African Literature Studies. uk 171-188.

Mungai, C. (2017). As a society, we have failed to inculcate reading culture at youth stage. Katika Standard Digital. https://www.standardmedia.co.ke/business/article/20011228119/as-a-society-we-have-failed-to-inculcate-reading-culture-at-youth-stage Tarehe 24/8/2019, 5:10 PM.

Obama, B. (1995). Dreams from my father. New York: Times Books.

Paneli la Kiswahili. (2018). Wasifu. Katika http://swa.gafkosoft.com/wasifu

Robert, S. (1936). Maisha yangu na baada ya miaka hamsini. Tanga: Mkuki wa Nyota Publishers.

Robert, S. (1958). Wasifu wa Siti Binti Saad: Mwimbaji wa Unguja. Tanga: Mkuki wa Nyota Publishers.

Robert, S. (1991). Wasifu wa Siti Binti Saad. Mkuki Nyota Publishers. Katika http://www.africanbookscollective.com/books/wasifu-wa-siti-binti-saad. Tarehe 18/8/2019 4:55PM

Rollins, J. D. (1983). "A history of Swahili prose: Part one from the earliest times to the end of the nineteenth century". Leiden: Brill Academic Publishers.

Sachdev, N. (2019). Report: Ebooks for building healthy reading habits among Africa's youth. Katika https://allafricayouth.com/2019/02/27/report-ebooks-for-building-healthy-reading-habits-among-africas-youth Tarehe 24/8/2019 5:55PM

Shafi, A. (2010; 2013). Mbali na nyumbani. Dar es salaam & Nairobi: Mizizi & Longhorn

UNESCO. (2016). Education recommendations in Latin American Terce: Third Regional Comparative and Exploratory Study. Katika http://www.unesco.org/new/fileadmin/MULTIMEDIA/FIELD/Santiago/pdf/Education-Policies-Recommendations.pdfTarehe 26/8/2019: 11:38 PM

Walibora, K. (2014). Nasikia sauti ya mama. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (1992)."Nagona and Mzingile. Kezilahabi's Metaphysics. KISWAHILI VOL. 58. Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam, Tanzania.". Katika Proceedings of the African Regional Symposium on Biotechnology for Rapid Development ,Nairobi, Kenya, 17th - 21, February, 1992. pp 233-239. Bull. Environ. Contam. Toxicol; 1991 https://profiles.uonbi.ac.ke/wadi/publications/nagona-and-mzingile-kezilahabis-metaphysicskiswahili-vol-58-institute-kiswahili-r

Wamitila, K. W. (2003). Kichocheo cha fasihi: Simulizi na andishi. Nairobi: Focus Books.